**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

# HOTUBA

**YA**

**MHE. HAMZA SAIDI JOHARI**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YA KUFUNGA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

**UKUMBI WA MIKUTANO WA SHULE YA UONGOZI YA MWALIMU NYERERE KIBAHA MKONI PWANI**

**24 JANUARI, 2025**

- **Bw. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bw. Edward Selya, Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu;**
- **Bw. Hassan Nkya, Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Bi. Zella Kiliat Lwemanyila, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Mwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi,**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana;**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA …**

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI …**

**Watumishi wenzangu na wajumbe wa Baraza,**

Nami niungane na viongozi wengine waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo katika Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninawashukuru wajumbe wa Baraza na wote mliotenga muda wenu kuja katika kikao hiki.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuratibu na kuandaa kikao hiki. Nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawashukuru wajumbe wa Sekretarieti kwa kazi kubwa waliyoifanya ya maandalizi ya kikao hiki. Hongereni sana.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kukutana na wajumbe wa Baraza hili, nimefurahi sana kuona tumefikia hitimisho la Mkutano huu kwa mafanikio makubwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Natambua kuwa, kikao hiki cha Baraza kimetanguliwa na mafunzo kwa viongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nilitamani sana kushiriki katika mafunzo hayo lakini kutokana na mwingiliano wa majukumu sikuweza kushiriki. Nimefahamishwa kuwa mafunzo yametolewa kwa siku 4 kuanzia tarehe 20 mpaka 23 Januari, 2025. Ni

imani yangu kuwa viongozi wote mliobahatika kuhudhuria mafunzo hayo mtaleta mabadiliko chanya kwenye Ofisi yetu na nchi kwa aujumla kwa kutoa huduma bora za kisheria.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Nimesikiliza kwa makini taarifa mbalimbali na hoja zilizowasilishwa siku ya leo na nimeamini kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inawatumishi wachapakazi, wenye bidii na moyo wa kujituma. Michango

mliyoitoa inadhihirisha kuwa mnadhamiria kuitekeleza kauli mbiu yetu ya ***“Weledi na Ubora”*** kwa vitendo. Ninashukuru sana kwa michango yenu muhimu, ambayo kwa hakika imechochea mjadala wetu.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali amewasilisha Risala yake ambayo imeeleza kwa kina kazi mbalimbali zilizotekelezwa na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Baada ya kusikiliza Risala hiyo nimebaini kuwa, masuala yaliyoelezwa ni muhimu sana ambayo kwa namna moja au nyingine yanachochea kuboresha maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Yale yote niliyoahidi kuyatekeleza nitayatekeleza hususan suala la kuboresha mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Mkurugenzi wa Mipango ametupitisha katika taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2025 na maoteo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo pia imeelezwa katika Hotuba ya Makamu Mwenyekiti wa

Baraza. Kwa kifupi, masuala yote yaliyoelezwa humo ni matokeo ya bidii ya kufanya kazi mliyonayo. Nawasihi muendelee na moyo huo.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Pia tumepokea taarifa ya Hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka kwa Mhasibu Mkuu na hoja mbalimbali kutoka katika Divisheni, Vitengo na Ofisi za Mikoa. Kwa kiasi kikubwa hoja zilizoibuliwa katika taaarifa hizi zinaeleza changamoto ambazo zinatukabili kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambazo zinapaswa kutatuliwa na sisi wenyewe ama kwa kushirikisha wadau wetu mbalimbali.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Hotuba ya mgeni rasmi inatuasa sisi watumishi tufanye kazi kwa bidii wakati tukiendelea kutatua changamoto zinazotukabili. Wakati nikitoa hotuba yangu ya kutoa mwelekeo wa dira ya OMMS niliwaeleza kuwa **“kabla hujajua unapokwenda, unapaswa kujua mahali ulipo”**. Naamini mpaka sasa kila mmoja wetu anajua mahali tulipo. Ni vema tuendelee kuchapa kazi kwa bidii ili tuweze kufikia dira yetu. Ni imani yangu kuwa ipo

siku tutafanya maadhimisho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kusherehekea mafanikio tuliyoyapata tokea Ofisi hii ilipoanzishwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Sisi sote tunalo jukumu la kuweka msingi imara wa kutimiza ndoto hiyo. Tunapaswa kuonyesha uongozi thabiti, dhamira na kujitolea bila ubinafsi na kufanya baadhi ya maamuzi magumu ili kuhakikisha tunaboresha maisha bora ya sasa na baadaye kwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Nimebaini katika kipindi kifupi nilichoongoza Ofisi hii ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushindwa kutumia rasilimali watu na mali zilizopo kuleta mabadiliko katika Ofisi. Changamoto nyingine kubwa niliyoibaini ni kuchelewa au kutotoa mrejesho kwa wakati kwa wadau wetu. Aidha, kuna baadhi ya watumishi hawazingatii sheria, taratibu na Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma katika kutoa huduma kwa wateja wa ndani na nje.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Katika hotuba ya mgeni rasmi alitaja jambo moja la msingi sana ambalo ni muhimu kwetu kulizingatia ili tuweze kuongeza uwezo wetu wa kifedha wa kitaasisi kwa kutumia huduma tunazozitoa. Tunamshukuru sana mgeni rasmi kwa kutukumbusha jambo hilo muhimu. Ndoto na matarajio yetu iwe ni kufanya mabadiliko katika kipindi cha uongozi wetu na kushughulikia changamoto zilizopo.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Katika jitihada za kutatua baadhi ya changamoto nilitoa pendekezo la kuundwa kwa Vikao vya Kitaalamu vya menejimenti (Menejiment Technical Committee) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ambayo yanahitaji kujadiliwa kwa kina na kutolewa ushauri wa kisheria ambao ndio utakuwa msimamo wa Serikali. Vikao hivi vinaendelea kufanyika kila wiki na kila mwezi na mpaka sasa tumeweza kutatua changamoto kadhaa za kisheria ambazo zilikuwa zinahitaji kufanyiwa maamuzi ya pamoja baada ya kuchakatwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Aidha, nimeshafanya ziara katika Ofisi za mikoa ya Mwanza, Mtwara na Arusha na kubaini kuwa changamoto kubwa inayowakabili *Regional State Attorneys* ni ufinyu wa Ofisi, vitendea kazi, magari na hata upungufu wa watumishi. Nitaendelea kufanya ziara katika Ofisi zote za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizopo mikoani kwa lengo la kubaini rasilimali tulizonazo ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili Mawakili wa Serikali wanaotuwakilisha katika mikoa ili tuweze kuzipatia ufumbuzi.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Leo nimefikisha siku **163** tokea nilipoteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Natambua kuwa Ofisi hii ni ya muda mrefu hivyo baadhi ya majengo yake ni chakavu na mengine yanahitaji kufanyiwa ukarabati wa kina. Kutokana na ushirikiano mzuri tulionao, wadau mbalimbali wametusaidia kufanya ukarabati mdogo na kuweka Samani za Ofisi mpya katika baadhi ya Ofisi zilizopo katika jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lililopo Dar es Salaam na ukumbi wa mikutano. Nitaendelea kufanya ukarabati katika Ofisi mbalimbali kadri fedha zitakavyopatikana na baadhi ya wadau wameahidi kutupatia Samani za Ofisi.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Kama alivyosema Makamu Mwenyekiti wa Baraza katika hotuba yake, Nami niwaahidi kuwa, tutaendelea kupandisha motisha za watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwaongezea mishahara na kuwalipa posho mbalimbali. Kuhusu maboresho ya muundo wa Ofisi, mapendekezo yaliyotolewa katika kikao hiki ni ya muhimu sana yakazingatiwe.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Jitihada kubwa zinapaswa kufanyika ili nyumba za viongozi ziweze kurejeshwa au kumilikishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kufanyiwa ukarabati kabla ya kuanza kutumika. Kwa maeneo ambayo yanachangamoto ni vema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iangalie namna bora ya kutatua changamoto hizo kwa kufanya mazungumzo au majadiliano na Taasisi husika ambayo hayataingiza Serikali gharama kubwa. Natumaini ushauri huu utawasilishwa katika kikao cha menejimenti kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Baada ya kusema hayo na kwa kuzingatia maazimio ya kikao hiki natoa maelekezo yafuatayo:

(a) Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waweke kipaumbele kwa kutenga fedha kwa ajili ya kununua vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi ndani na nje ya nchi;

(b) Kila Divisheni na Kitengo iende kutekeleza maazimio yote yaliyotolewa katika kikao hiki au kujiwekea mkakati ya namna bora ya kukamilisha utekelezaji wa maazimio hayo. Mwisho wa Mkutano huu utakuwa ni mwanzo wa utekelezaji wa yale ambayo tumeyazimia kuyatekeleza pamoja baada ya kurudi katika vituo vyetu vya kazi. Ni imani yangu pia kwamba kila mmoja wenu kupitia mafunzo yaliyotolewa kwa muda wa siku nne ameongeza maarifa mapya na hivyo kuwa na ari na nguvu mpya ya kufanya kazi kwa juhudi, maarifa, ubunifu na kuendelea kubadilishana uzoefu pale itapobidi; na

(c) Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu iendelee kuhakikisha inalinda mali za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama vile viwanja na majengo mbalimbali ya Ofisi kwa kutafuta Hati za Umiliki wa maeneo husika.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Ujumbe wangu wa leo kwenu unasema:

***"DO WHAT YOU CAN, WITH WHAT YOU HAVE, WHERE YOU ARE"***

***“BAD DECISION, MAKE GOOD STORIES”***

***“TOUGH TIMES DONT LAST, TOUGH TEAMS DO”***

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

Nimalizie kwa kutoa tena shukrani zangu kwa wote walioandaa Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawatakia safari njema wote mtakaosafiri kurejea katika vituo vyenu vya kazi. Baada ya kusema hayo, sasa natamka rasmi kuwa Mkutano huu wa

Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umefungwa rasmi.

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI …**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**

Hamza S. Johari
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**